Toleo 73 - Rajab 1444 H / Februari 2023 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Nidhamu Mbovu ya Kijamii ya Kibepari ndio Kiini cha Machafu ya Kijamii

**HABARI NA MAONI**
Wakati wa Enzi ya Watawala Waovu, Matukufu ya Uislamu Yanakiukwa

**MATOLEO**
Wako wapi Wanaume?

**JIBU LA SWALI**
Habari ya Upokezi wa Mmoja Mmoja (Khabar Ahaad) Yalazimu Kufanyiwa Kazi



**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 05/1444 | Ijumaa, 27 Jumada II 1444 H | 20/01/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Nidhamu Mbovu ya Kijamii ya Kibepari ndio Kiini cha Machafu ya Kijamii

Utafiti wa serikali wa hivi karibuni umefichua kusheheni pakubwa mahusiano ya nje ya ndoa ambapo inatajwa kuwa wanaume walioko kwenye ndoa wanatoka nje ya ndoa zao kwa kuwa na wapenzi saba huku wanawake nao wakiwa na wapenzi wawili. Aidha, utafiti huu ukadokeza majimbo yanayoongoza katika visa vya kwenda nje ya ndoa.

**Kwa haya, sisi katika Hizb ut-Tahrir Kenya tungependa kubaini yafuatayo:**

Chini ya mfumo wa Kisekula na fikra za Kiliberali, uzinzi, uasherati na ukahaba na mengine mengi machafu huwa ni yenye kukubalika kijamii, kitamaduni na hata kikanuni. Usekula hubeba fikra finyo za uhuru wa kibinafsi na uhuru wa kujumuika ambao huwa ndio nishati inayosukuma watu kujihusisha na mahusiano ya nje ya ndoa zao pasina na kuwa na hata chembe ya haya. Kwa maana hii, ndani ya mazingira haya machafu, mahusiano ya nje ya ndoa ni mojawapo ya majanga ya kifamilia.

Mfumo wa Kijamii wa Kirasilimali umeharibu ndoa kwa utaratibu, umeharibu uzazi, na kuchochea kuvunjika kwa utengamano wa Familia. Katiba za kilimwengu pia zimeshindwa kutangaza waziwazi uhalifu wa uzinzi na ukahaba ambao ni biashara inayofanywa peupe ndani ya tawala za kisekula. Zaidi ya hayo, sheria ya Kimataifa ya haki za binadamu inawapa wanaharakati kama vile wanaharakati wanaotetea haki za wanawake mfumo dhahania wa kutetea kikamilifu maovu haya hivyo kuushambulia Uislamu ambao umeharamisha zinaa na kuutaja kuwa ni njia mbovu.

Nidhamu ya Kijamii ya Kiislamu imeweka misingi inayolenga kuunda jamii yenye mtazamo sahihi wa mahusiano baina ya wanaume na wanawake unaolenga matangamano mema baina ya jinsia hizo mbili ukiwaongoza katika kulinda heshima yake. Kwa hiyo, pamoja na utekelezaji wa kidhati na utekelezwaji wa maadili na sheria za taratibu ya kijamii ya Kiislamu, mtazamo wa jamii kuhusu uhusiano kati ya wanaume na wanawake uko mbali na kushinikizwa na kipengele cha maingiliano tu ya kimwili na starehe. Zaidi ya hayo Uislamu umeharamisha uzinzi na matendo yote machafu. Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

﴿وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنَا إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا﴾

**“Wala msikaribie Zina. Hakika huo ni uchafu na ni njia mbaya kabisa.”** [Al-Isra: 32]

Uislamu ndio mfumo uliofanya uchajimungu uwe ndio nishati ya mtu inayompelekea kujizuia sio tu na uzinifu bali machafu yote kwa ujumla. Sheria ya Kiislamu imewajibisha wanaume na wanawake kujipamba na sifa ya haya inayowafanya wajiepushe na kila ovu bali wajifunge kikamilifu na sheria za Mwenyezi Mungu zinazoambatana na maisha yao ya kijamii. Katika Uislamu, ndoa hufungwa kwa lengo la kutafuta stara, kukidhi hisia za kimwili ili kuwe na utulivu huku ikiangaliwa zaidi kama njia itakayoletea mafanikio makubwa ya kijamii.

Kuzuia na maovu haya ya kijamii, jamii inapaswa kukataa hulka na mawazo finyo ya kiliberali yanayolinganiwa na Urasilimali na siasa yake ya Kidemokrasia. Wanapaswa pia kufanya kazi ya kuusimamisha Uislamu na mfumo wake wa utawala nao ni Khilafah kwa njia ya Utume.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut-Tahrir Kenya**

Afisi ya Habari Kitengo cha Wanawake

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 25/1444 Jumapili, 1 Rajab 1444 H 22/01/2023 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir Chazindua Kampeni ya Kimataifa:

# "Mabadiliko Halisi ni kwa kupitia Ulinganizi wa Khilafah PEKEE"

Leo, ulimwengu uko katika machafuko na giza, karibu na mbali. Mateso na taabu za wanadamu zinaongezeka siku hadi siku huku mataifa yakiingia kwenye mgogoro mmoja hadi mwingine. Umaskini, utovu wa usalama wa kifedha, njaa, mauaji ya halaiki, uvamizi wa kikatili, udikteta, vita vya kinyama, kuvunjika kwa familia, maisha yenye uharibifu, milipuko ya uhalifu, unyanyasaji dhidi ya wanawake, matatizo ya afya na elimu na matatizo mengine yanayolemaza yanakumba nchi kote ulimwenguni, chini ya mifumo ya kibinadamu iliyoharibika na uongozi mtepetevu ambao haujui jinsi ya kuchunga ipasavyo mambo ya watu wao na kutimiza mahitaji yao. Badala yake sera, sheria na matendo yao yanazidisha mateso ya watu wao.

Ardhi za Kiislamu na dunia hazistahili ziwe katika hali hii ya giza, uharibifu, majanga na migogoro inayoonekana kutokuwa na mwisho. Hata hivyo, mabadiliko ya halisi hayawezi kufikiwa kwa kufanya mabadiliko madogo madogo kwa mifumo yenye dosari ambayo inatabikishwa kwa sasa, au mabadiliko ya hatua kwa hatua – kurekebisha tu ubavu wa matatizo, au kutoa ufumbuzi wa plasta ya kunata, au kurudisha mzunguko wa mifumo ya kidemokrasia ya kisekula iliyofeli kwa nyuso mpya kwenye usukani - mifumo ambayo imethibitisha mara kwa mara, kutokuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya wanadamu, kuwalinda wanaodhulumiwa au kutoa haki - na inadumisha tu ahadi ya kurefusha machungu na mateso ya Umma wa Kiislamu na wanadamu.

Mabadiliko halisi yanatuhitaji sisi kama Waislamu kukumbatia ruwaza zaidi ya hali ilivyo sasa, mfumo wa sasa wa kibepari wa kiulimwengu, mifumo ya sasa iliyobuniwa na mwanadamu. Inatuhitaji kuinua macho yetu juu ya njia mbovu na angamivu za kutawala na kuendesha mambo yetu tunayoyaona yametuzunguka. Inahitaji mabadiliko makubwa, ya msingi na mapana. Inahitaji kuzaliwa kwa mfumo badali unaobeba masuluhisho halisi kwa matatizo ya binadamu. Inatutaka sisi kama Waislamu kuregea katika yale ambayo Mwenyezi Mungu (swt) ametuitia kwayo - Sheria Zake, Mfumo Wake, na kuutabanni ujumbe wetu wa Kiislamu, ili kusimamisha uongozi wa kweli kwa wanadamu: Khilafah kwa Njia ya Uislamu. Ni Mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt) pekee ndio utakaoleta mafanikio kwa Ummah huu na kwa wanadamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**[فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم مِّنِّي هُدًى فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَى * وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى]**

**"Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika. Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu."** [Ta-Ha: 123-124].

Rajab hii, mwezi unaoadhimisha mwaka wa 102 wa kukosekana kwa Khilafah, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir kitazindua kampeni ya kimataifa yenye kichwa: "Mabadiliko Halisi ni kwa Kupitia Ulinganizi wa Khilafah PEKEE". Itachunguza maoni ya sasa kuhusu jinsi mustakbali mwema zaidi unavyoweza kupatikana kwa ardhi za Kiislamu; jinsi Khilafah itageuza machafuko kuwa mwamko kwa kanda hiyo na jinsi inavyobeba masuluhisho halisi kwa matatizo ya wanadamu; na pia itajadili dori ya Waislamu katika kuleta mabadiliko halisi katika ulimwengu wa Kiislamu na kimataifa; na kama mabadiliko msingi na kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume ni ndoto au inawezekana kweli. Kampeni hii inaweza kufuatiliwa kwenye: www.hizb-ut-tahrir.info na ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/womenscmoht. Link ya video ya utambulishaji wa kampeni: https://youtu.be/zRk5dx2t1ew

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Wakati wa Enzi ya Watawala Waovu, Matukufu ya Uislamu Yanakiukwa

**Habari:**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Mevlüt Çavuşoğlu, alisema kuwa kuitwa kwa balozi wa Uswidi jijini Ankara mnamo tarehe 22 Januari 2023, kulijiri kama kulaani dhidi ya kuchomwa moto kwa Qur'an Tukufu mbele ya jengo la ubalozi wa Uturuki jijini Stockholm. Çavuşoğlu ameongeza kuwa, balozi wa Uturuki jijini Stockholm alikutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uswidi, Tobias Billström, na kumfahamisha kuhusu kutoridhika kwa Uturuki, na kukataa kwa serikali ya Uswidi kuwaruhusu waandamanaji kuchoma Qur'aniTukufu mbele ya jengo la ubalozi wa Uturuki.

Alieleza kuwa kuchoma Qur'an Tukufu na uadui kwa Uislamu na Waislamu hakuingii ndani ya uhuru wa kibinafsi. Serikali za Magharibi haziruhusu uchomaji wa vitabu vitakatifu vya dini nyenginezo. Ama Waislamu na matukufu yao, haraka wanahalalisha hilo kwa uhuru wa kujieleza. Çavuşoğlu alidokeza kuwa hakuna maandishi katika katiba ya Uswidi, wala ndani ya sheria za Muungano wa Ulaya, yanayoonyesha kuwa kuchoma Qur'an Tukufu iko chini ya uhuru wa kujieleza. Aliendelea, "Licha ya maonyo yetu yote, mamlaka za Uswidi zilitoa ruhusa ya kuchomwa Quran Tukufu, na hii inachukuliwa kuwa ni uhalifu dhidi ya Uislamu na Waislamu kote duniani."

Pia ameashiria kuwa jamii ya Waturuki jijini Stockholm itaandaa maandamano mbele ya jengo la ubalozi wa Uturuki, na kuashiria haja ya serikali ya Uswidi kuchukua hatua zinazohitajika ili kuzuia kutokea tena kwa uhalifu kama huo.

**Maoni:**

Katika zama za Erdogan na Çavuşoğlu, Qur'an Tukufu imekuwa ikichomwa moto mara kwa mara, huku matusi dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na Uislamu yakiongezeka. Hata hivyo, tunasikia tu maandamano na lawama kutoka kwa watawala hawa! Je, munadhani hili ndilo jibu sahihi kwa vitendo hivyo?! Lau Suleiman Mtukufu angekuwa hai, majibu yangekuwaje? Kama Mu'awiyah bin Abi Sufyan angekuwa hai, majibu yangekuwaje? Kama Omar bin Abdul Aziz angekuwa hai, majibu yangekuwaje? Kama al-Hajjaj angekuwa hai, majibu yangekuwaje?

Wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), Yahudi mmoja alimshambulia mwanamke Muislamu, na jibu lilikuwa ni kufukuzwa kwa Mayahudi wa Banu Qaynuqa' kutoka Madina. Wakati wa Al-Mu'tasim, mwanamke Muislamu alivamiwa, hivyo Amuriyya ilitekwa. Wakati wa Hajjaj, wanawake wa Kiislamu walivamiwa, na baadhi yao walitekwa, hivyo Sindh na Hind zilifunguliwa.

Ama zama za watawala hawa wa sasa, waovu, Palestina ilipotea, na watawala hawa wakakimbilia kusawazisha mahusiano na Mayahudi, huku mauaji ya kishahidi ya Waislamu yakiwa ni jambo la kawaida, bila aibu. Kila siku, Mayahudi wanawaua shahidi vijana wa Kiislamu, huku hakuna mtawala yeyote anayenyosha kidole, sio hata kwa kiwango cha maneno ya kukashifu, kulaani na kupinga.

Wakati wa Suleiman Mtukufu, Suleiman alituma mjumbe kwa Mfalme wa Hungary, na Mfalme wa Hungary akamuua mjumbe wake. Suleiman Mtukufu aliongoza jeshi kibinafsi na kuifungua Belgrade, mji mkuu wa Hungary, katika mojawapo ya vita vikali zaidi katika historia, Vita vya Mohács.

Ama wakati wa Muawiyah bin Abi Sufyan, wakati jeshi la Waislamu lilipokuwa likiizingira Konstantinopoli, Abu Ayyub al-Ansari aliomba azikwe karibu na ukuta wa Konstantinopoli, na kwa hakika alizikwa kwenye sehemu ya karibu zaidi ya ukuta. Kaisari wa Rumi alijulishwa juu ya hilo, hivyo akatangaza kwa Muawiyah kwamba atalifukua kaburi na kuitoa ile maiti kwa ajili ya mbwa. Basi Mu'awiyah akamtangazia Kaisari wa Rumi, **"أقسم بالله لو أن يدا امتدت إلى القبر لما تركت نصرانيا في بلاد المسلمين إلا قتلته، وما تركت كنيسة إلا هدمتها"** "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, lau mkono utarefushwa kwenye kaburi sitamwacha Mkristo hata mmoja katika nchi za Kiislamu bila ya kumuua, na sitaacha kanisa hata moja, bila ya kulibomoa." Kisha Kaisari wa Warumi akaamuru watu wake walilinde kaburi wao wenyewe, kwa kuogopa kwamba mmoja wa watu wa Kirumi anaweza kulifukua kaburi hilo!

Hivi ndivyo ardhi muitiko wenye mtingisho wa dunia lazima uwe, sio kwa maandamano, bali kwa majeshi yanayowatiisha maadui!

Kwa kumalizia, tunasema kuwa Khilafah ni ngao ya Uislamu na Waislamu. Wakati Khilafah ilipovunjwa, watu waovu zaidi waliushambulia Uislamu na Waislamu. Lau watawala wa kikafiri wangejua kwamba kuna mtawala katika Ardhi za Kiislamu anayekamata haki kwa mikono yake mwenyewe, wangeiweka Qur'an Tukufu juu ya sahani ya dhahabu, na kuiinua juu ya vichwa vyao...

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Muhammad Salim – Ardhi Iliyobarikiwa (Palestina)**

# Wako wapi Wanaume?

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



Mwanachuoni, Sayyid Qutb, katika kitabu chake kwa jina, "Katika Kivuli cha Qur'an" kuhusiana na aya: وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَـٰٓئِكَةِ إِنِّى جَاعِلٌ فِى ٱلْأَرْضِ خَلِيفَةً **"Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia malaika, 'Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi).'"** [Al-Baqarah: 2:30] Alisema kwamba zipo fahamu na mazingatio msingi mawili kuhusiana na mwanadamu kama bwana wa ardhi ambayo ni kama ifuatavyo:

Kwanza – mwanadamu ni bwana juu ya ardhi; kila kitu kimeumbwa kwa ajili ya manufaa na furaha yake. Hili humnyanyua mwanadamu juu ya viumbe vingine na huharamisha kumkandamiza na kumfedhesha kwa ajili tu ya maendeleo ya kimada. Ubinadamu wa mwanadamu lazima uheshimiwe na kulindwa; hakuna katika haki zake msingi au maadili hutakiwa kukiukwa au kuharibiwa kwa sababu yoyote ile. Vitu vya kimada vipo kwa ajili ya kumtumikia mwanadamu na vimetengenezwa kwa ajili ya kupiga jeki ubinadamu wake na kuboresha uwepo wake. Hivyo basi, haingii akilini kwamba maendeleo yake yapatikane kwa kulipa gharama ambayo itatishia maadili yake, heshima na hadhi yake.

Pili – dori ya mwanadamu ardhini ni ya umuhimu mkubwa. Mwanadamu, na wala sio njia za uzalishaji au usambazaji, ndio nguvu ya kuleta mabadiliko ardhini; yeye hushawishi na kubadilisha mambo yote katika uhai wa ardhini. Kinyume na mtazamo wa kimadaniya, mwanadamu ndio bwana, na sio mtumwa wa mashini.

Kwa kuongezea, mwanachuoni na muasisi wa Hizb ut Tahrir, Sheikh Taqiuddin an-Nabahani, asema katika kitabu chake, *Kufikiri (At-tafskir)*: Mwanadamu ndiye kiumbe pekee kilicho fadhilishwa zaidi; hata kiasi kwamba imesemekana – ambako ni kweli – kwamba amefadhilishwa zaidi kuliko malaika. Akili (*'aql*) ya mwanadamu ndiyo iliyo nyanyua cheo chake, na kumfanya kuwa juu ya viumbe vyote.

Dunia hivi sasa inasumbuka na imezama katika fujo. Kila mmoja anaotesha vidole na kuwalaumu wanawake kuwa ndio chanzo cha machafuko ya kijamii kama kuzidi kwa viwango vya talaka, kuvunjika kwa familia, na kuwepo kwa watoto wakorofi miongoni mwa maovu mengine. Kiupande wa kiuchumi, wanawake wanalaumiwa kuwa wameweka kipaumbele ajira zao na kuleta mashaka katika sekta ya uajiri kwa kutoa huduma kwa bei duni na wanapatikana kwa wepesi kutoa nguvu zao kwa waajiri walafi. Kwa upande mwingine, wanawake sasa wanashindana na wanaume katika kupanda ngazi za kisiasa. Kwa kifupi, wanawake wapo katikati wakibeba lawama zinazochipuza kutoka kwa wanaume duniani kote.

Hakika, ukweli ni kwamba wanawake ni wahanga wa wanaume waliofeli kuitikia na kubeba majukumu kama ilivyotarajiwa sio tu na Shari'ah ya Kiislamu, bali hata asili ya maumbile ya kiume. Mwanamume kiasili anacheza dori ya kiongozi na mwenye mamlaka juu ya

***Endelea... UK 6***

viumbe vingine. Hivyo basi, mwanamume lazima awe na lengo / misheni ya kwa nini yupo katika dunia hii ya muda mfupi. Kwa kuongezea, lazima awe na maarifa ya kidharura kuhusiana na lengo lake na namna ya kulitimiza. Misheni ya mwanadamu hapa katika dunia ya muda mfupi imefupishwa katika aya hii,وَمَا خَلَقۡتُ ٱلۡجِنَّ وَٱلۡإِنسَ إِلَّا لِيَعۡبُدُونِ **“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.”** [Adh-Dhariyat: 51:56]. Kumwabudu Mwenyezi Mungu (swt) kunamaanisha kujisalimisha kwa maagizo Yake kwa maana kujifunga na maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake pasina kuzingatia natija (madhara au manufaa) inayotoka kwayo.

Kwa hivyo, mwanadamu anaposonga mbele katika maisha kama mtumwa wa matamanio yake basi bila shaka tunatarajia maisha ya majanga na watu kuzama katika vina vya chini katika ufuska na kutobeba majukumu. Katika jamii ya leo, hatuko salama kutokamana na mporomoko wa kisiasa, kijamii, kiuchumi na kielimu. Mwanamume, kama kiongozi amefeli kuitumia akili yake kutafuta njia sahihi kumuelekea Muumba wake; hivyo basi amedumu katika kazi za kubahatisha kwa kisingizio cha uhuru usiokuwa na mipaka! Na kupelekea meli (familia) kuendelea kuzama ndani zaidi kwa sababu mwanamume, kama nahodha, hana lengo na ruwaza!

Wanaume wa karne ya ishirini na moja wamepoteza uume wao! Ni watumwa wa matamanio yao kiasi kwamba wamekuwa vipofu na hawaioni dori ya uume waliotwikwa na Mwenyezi Mungu (swt). Kidhati, wameikana dori yao ya uongozi na badala yake wamemakinisha akili na muda wao katika kuzifukuzia starehe zisizoeleweka, hadaifu na za kilafi za ulimwengu huu wa muda mfupi huku hawazingatii mahangaiko na mdororo wa kisiasa, kijamii, kiuchumi na kielimu duniani kote.

Ala! Sio jambo la kushangaza kuwashuhudia wanaume leo ambao hawawezi kuwakidhia familia zao mahitaji msingi. Hata hivyo, watu hao hao wanaweza kumudu kununua simu za mkononi au vifaa vya kidijitali vya kisasa ambavyo vina thamani ya mahitaji msingi ya miezi miwili kwa ajili tu ya kuonekana kuwa wanakwenda na wakati ndani ya jamii. Badala ya kujenga maktaba ya nyumbani na kuijaza vitabu adhimu ambavyo vitaziimarisha familia zao, baadhi ya wanaume wanashindana na kujifahiri katika kununua runinga kubwa au vituo vya michezo vya kisasa kwa familia zao! Wanaume wa zama zetu wamezama katika upuzi na mambo duni kwa sababu hawana misheni au ruwaza; daima wanapiga miayo na wana njaa ya anasa zinazofuata. Wanaume wametingwa na shughuli zao ilhali wanawake, watoto na wazee wamesakamwa na machozi ya kukata tamaa baada ya kutaka msaada ambao hawaupati! Wanaume wamesalimu amri ndani ya nyumba zao (meli) na hivyo basi wanachama wa familia (abiria) kila mmoja amejimakia!

Ala! Haingii akilini kuwaona wanawake wakiitikia na kuchukua silaha ili kujikomboa kutoka kwa makucha ya madhalimu kama Bashar al-Assad nchini Syria. Kwa upande mwingine, wanaume wanashughulika kupiga njama ili kuubakisha mamlakani utawala huo huo! Wanaume wa zama zetu hawakuisaliti jamii tu bali hata afya zao wenyewe! Inakuwaje mwanamume kuwa na tumbo kubwa huku akiwa na majititi yote kwa kisingizio kuwa ni ishara ya kufaulu kwake ndani ya jamii! Siku hizi imekuwa vigumu kutofautisha baina ya mume na mke, nani kati yao anakaribia kujifungua? Kwa sababu wote daima wamenenepa na kuchoka! Kinyume chake, wanaume ni wembamba nje na wanene ndani (TOFI). Kuna jambo haliko sawa, na wanaume wanatakiwa kuzinduka kutoka usingizini na kuchukua uongozi. Wasipofanya hivyo, mambo yalivyo sasa lau yatabakia hivyo pasina kushughulikiwa, basi janga la kiafya lililoko mbele yetu litakuwa ni tone baharini tukilinganisha na linalo kuja!

Hayo hapo juu ni taswira tu ya hali ya kutamausha inayoikumba dunia leo. Ni kutokamana na kufeli kuwalea wanaume wa kweli ili kubeba dori ya uongozi na kuiongoza dunia. Jamii leo inawalea vijana wa kina mama ambao wanakuwa na kuchukua nyadhifa za uongozi na kuendeleza tabu za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kielimu zinazoshuhudiwa leo!

Wakati ni sasa kuwalea na kuwakuza wanaume wenye ikhlas ambao watakuwa Waislamu wanachuoni, watawala na wanajeshi katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt) ma Mtume Wake (saw). Wanaume ambao hawataogopa lawama kutoka kwa yeyote: Wanaume ambao watakuwa tayari kuhimili shinikizo zozote zinazochipuza kutoka kwa wale walio na akili dhaifu miongoni mwa watu: Wanaume ambao hawana muda kushiriki usengenyaji: Wanaume ambao viwango vyao vya akili tambuzi viko juu katika kutekeleza haki kwa yeyote pasina kujali kabila, rangi, hali ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kielumu: Wanaume ambao wako tayari kufanya biashara na uhai wao ili kununua Jannah kwa ajili ya kuilinda hadhi ya Mtume Muhammad (saw) na ujumbe wake: Wanaume walio tayari kutupilia mbali hali zao za utulivu na kujitosa katika vina vya chini katika kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw) katika lile linalopeana uhai: Wanaume walioweka kipaumbele utafutaji wa Akhera na kuyakimbilia yale yote ambayo yatatilia shime juhudi zao kutimiza lengo lao hilo.

Suali msingi ni wako wapi wanaume? Hakika, wanaume wapo, bali tunapolitizama na kulichanganua suali kwa mtizamo wa kijuujuu, itamaanisha wanaume waliovalia suruali au kanzu za Waislamu n.k. Hata hivyo, tunapozama ndani na kulitathmini suali kwa kina, linatuchochea ili kutafakari hali iliyoko sasa ya wanaume wetu. Lau kila mmoja wetu atajitafakari kwa kina atafikia uamuzi kuwa tupo hapa tulipo kwa sababu ya mawazo ya kisekula tunayo yabeba. Mawazo yetu huzalisha

***Endelea... UK 7***

fahamu zetu, nazo huepelekea kupatikana kwa vitendo vyetu. Hivyo basi, ili kubadilisha hali ya kutamausha iliyoko sasa ya wanaume duniani kote, ni lazima tujifunge na yafuatayo:

**Kwanza, kujifunza Shari'ah ya Kiislamu;** inayojumuisha kuisoma, kuielewa na kujifunga na Qur'an kama muongozo wa milele kwa wanadamu. Kwa kuongezea, lazima tuifahamu Sunnah (Hadith) kwa kuwa ni kiunga mkono na kipambanuzi cha Qur'an, kwa sababu vitendo vyetu vinatakiwa kuwa kwa mujibu wa Shari'ah ya Kiislamu. Na natija yake ni kuwa vitendo vyetu vikiifuata, basi itakuwa vinathibitisha utumwa wetu kwa Mwenyezi Mungu (swt) na huwa tunatarajia kupata huruma na radhi Zake. Mwenyezi Mungu (swt) asema, إِنَّمَا يَخۡشَى ٱللَّهَ مِنۡ عِبَادِهِ ٱلۡعُلَمَٰٓؤُاْۗ **"Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni.** [Fatir: 35:28]. Kwa kuongezea, Abu Hurairah amesimulia kwamba Mtume (saw) alisema, «مَنْ يُرِدِ اللَّهُ بِهِ خَيْرًا يُفَقِّهْهُ فِي الدِّينِ» **"Mwenyezi Mungu anapomtakia mtu khair, Humuwezesha kuifahamu dini."** [Sunan Ibn Majah].

**Pili, kujifunza elimu ya ziada inayohusiana na mambo msingi ya kimaisha;** ambayo itatusaidia katika kutekeleza shughuli zetu za kila siku katika maisha mfano kama kujifunza kuendesha gari n.k.

**Tatu, lazima tutenge muda wa kuwa faragha peke yetu;** kwa maana tutenge sehemu faragha kwa ajili ya kutafakari, kuitathmini thamani yetu na mchango wetu katika hali ya maisha ya familia na jamii zetu na taifa na dunia yetu kwa ujumla. Lazima tujiulize maswali kama: Mimi, familia na jamii yangu, na wanadamu kwa ujumla tupo katika njia ya sawa iliyo azimiwa na Mwenyezi Mungu (swt) au sisi ni mazumbukuku tunaofuata mkumbo?

**Nne, kujikurubisha na uchache;** daima kujisukuma kuwa mchache. Mtu mchache ni mtu ambaye ametosheka na kichache anachohitaji ili kukamilisa safari hii maisha ya muda mfupi. Mtume Muhammad (saw) aliongoza kwa mfano, licha ya kuwa ni Mtume na mtawala, aliishi maisha mepesi kabisa, mchache asiyekuwa na mfano. Lazima iwe wazi kwamba kuwa mchache sio sawa na kujibunia matatizo, bali kunamaanisha kila kilicho cha ziada unakiwekeza (unakitoa) kama sadaqah katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw). Hili linawezekana tu kupitia kujiuliza kiukweli, ni kiasi gani cha mali kinachotutosha katika mali tunazomiliki?

**Tano, kufunga mara kwa mara;** inamaanisha kwamba tule mlo mmoja au miwili kwa siku. Pia, twaweza kuigiza kufunga kwa Mtume Daud (as) kwa kufunga leo na kutofunga siku ifuatayo. Kwa upande mwingine, tunapofungua kiamshakinywa lazima tule **vyakula** na sio **bidhaa za chakula** ikimaanisha lazima tule vyakula ambavyo vinatunufaisha kwa virutubisho na SIO bidhaa za chakula zisizokuwa na virutubisho, bali huwa ndio chanzo cha kusababisha maradhi katika miili yetu. Kufunga mara kwa mara tena kwa muda mrefu hupelekea hali ya autofaji. Autofaji huruhusu miili yetu kuweza kuzisafisha seli za zamani katika miili na kuziwezesha kufanyakazi kwa ubora zaidi. Hii ni hatua ya kimaumbile ambayo huanza punde tu seli zetu zinapokosa au kunyimwa virutubisho.

**Sita, mazoezi ya mara kwa mara;** hususan ya kunyanyua uzani yanayojumuisha na kujulikana kwa lugha ya Kiingereza kama, 'bench press, deadlifts, overhead (ovh) shoulder press, squats na rows.' Kwa kuongezea, kushiriki mazoezi ya kasi mno kwa muda mfupi (HIITS) kama kukimbia mbio fupi. Kwa kifupi mazoezi ambayo yatahusisha tishu za misuli, ini, kongosho na mafuta ili kunufaika kiafya ya kiwiliwili, kiakili na kiujumla.

**Saba, kusoma vitabu daima;** itakusaidia kufikiri kwa umakinifu na ubunifu kwa kila suala utakalo kumbana nalo. Fauka ya hayo, kiwango chako cha kujiuliza maswali kitazidi na kukupelekea kuzidi kiu cha kutaka taarifa itakayo kupelekea kusoma zaidi. Imarisha uhai wa akili yako kwa kujenga maktaba ambayo utaitumia kama chemichemi ya kifikra ambayo utakuwa unairudia unapokwama juu ya baadhi ya masuala au unapotaka kupata msukumo au uchanganuzi juu ya suala lolote. KUMBUKA kitabu nambari moja kuwepo ndani ya maktaba yako ni Qur'an Kareem kisha vingine.

**Nane, sikiza audio au tizama video;** ambazo zinaongeza thamani yako na mchango wako kama mwanamume katika dori yako kama kiongozi wa familia, jamii na wanadamu kwa ujumla.

**Tisa, ilinde akili na muda wako;** hizi ndizo **rasilimali zako za KWELI** ambazo za kuhitajia kuwa na nidhamu, mpangilio na ujuzi ili kuweza kuzitumia ili kuweza kufikia kilele cha ufanisi. Kumbuka kwamba kila (mawazo) kinachoingia akilini mwako kitaamua utakavyokuwa. Ama kuhusu muda wetu, daima unakimbia dhidi yetu ikimaanisha kuwa hauwezi kupatikana tena, unapotoweka ndio umekwenda, lakini kila sekunde itahesabiwa na Mwenyezi Mungu (swt) Yaumul Nadama (Qiyama). Daima lazima tuufananishe ulimwengu na ubao, na katika mikono yetu, tunazo chaki zilizo fungamanishwa na wakati ambazo daima zinaandikwa kwa ajili ya kizazi chetu kijacho kutusoma. Andika uchafu na kizazi chako kitasoma hicho haswa!

**Kumi, jiunge na chama au kundi la watu** ambalo limejikita katika kuleta MAPINDUZI ya KWELI na ya KIMSINGI. Pamoja nao fanyakazi kuelekea lengo moja la kubadilisha hali mbaya iliyoko sasa ya wanadamu duniani kote. Hali ya maisha ya wanadamu itaboresheka kwa sharti kuwa chama kitajituma kurudisha maisha ya Kiislamu kwa msingi wa Shari'ah ya Kiislamu. Hivyo basi, lengo kuu la chama hicho lazima liwe ni kurudisha

***Endelea... UK 8***

tena Nidhamu ya Uongozi wa Kiislamu, Khilafah kwa njia ya Utume. Chama hichi si CHENGINE ISIPOKUWA ni Hizb ut Tahrir, (Chama cha Ukombozi). Chama kinacho fanyakazi usiku na mchana ili kumtoa mwanadamu kutoka katika minyororo ya utumwa kwa matamanio yake na kumrudisha katika utumwa wa Muumba wake – Mwenyezi Mungu (swt). Hizb ut Tahrir ina hamu ya kuwapata wanaume walio na afya imara, akili makinifu na wachapajikazi miongoni mwa wawajibikaji ili kuitikia mwito wake wa kusimamisha tena Khilafah.

Khilafah itatoa maana ya lengo na misheni kwa wanaume, ambao watachukia kupoteza muda wao katika kucheza kamare, kushiriki katika miamala ya riba, kutelekeza dori yao ya Jihad, nudu ya Uislamu. Wanaume watakaojiepusha na kujishughulisha na usengenyaji pamoja na wake zao au wanawake, ambao hawatolia kwa kuwa timu zao za mpira za kitaifa au vilabu zitakapofungwa! Watachukia wao kama waume pamoja na vijana wao, binti zao au wake zao kuzozana juu ya aina gani ya chakula wale, washangilie timu gani ya mpira ya kitaifa au kilabu au wazuru eneo gani kujiliwaza au kuvaa nguo gani katika harusi au tamasha la muziki lijalo?! Ewe Mwenyezi Mungu (swt) tusamehe kwa makosa yetu na upangaji wa kimakosa wa vipaumbele vyetu katika kizazi cha karne hii ya 21 kilichojikita katika mtazamo wa kimada!

Khilafah italeta vito kutokamana na wanaume kama vile Khalid bin Walid (ra) shujaa wa kiwango cha juu na kamanda mkuu asiyekuwa na mpinzani katika Jeshi la Waislamu huko Syria chini ya Khalifah (ra) Abu Bakr (ra). Sa'd bin Abu Waqqas (ra) shujaa makini wa kiwango cha juu na kamanda mkuu wa kijeshi huko Iraq chini ya Khalifah Umar bin Khattab (ra). Wanajeshi mahiri na wasiogopa kama Rib'i bin Amir (ra) waliofanya kazi chini ya usimamizi wa Sa'd bin Abu Waqqas. Rib'i bin Amir alikuwa mwanadiplomasia kwa Rustam, waziri wa vita wa dola ya Fursi. Yafuatayo ndiyo yaliyojiri:

*'Pindi yeye (Rib'i bin Amir) alipowasili katika makao ya Rustam, yaliyokuwa yamewekwa zulia la kitambaa cha dhahabu, mito ya hariri ya thamani, ilhali kiti cha kifahari chenye kito kiliwekwa katikakati. Rib'i bin Amir (ra) alikuja mpaka juu ya sakafu ya zulia hilo na kushuka juu ya farasi wake, akamfunga katika mto mmoja. Kisha akasonga mbele huku akiwa anasaidiwa na mkuki uliokuwa unadunga na kupasua zulia hilo na kulitia matundu kwa ncha yake, kisha kukaa mkabala na Rustam. Waliokuwepo walijaribu kumtoa katika kiti hicho cha kifahari na kumpokonya silaha zake. Hapo ndipo Rib'i bin Amir (ra) akatoa mngurumo, "Nimekuja kwa mualiko na sikujijia mwenyewe. Dini yetu inamkataza katakata mtu yeyote kukaa kama Mungu na wengine wasimame mbele yake ilhali wamefunga mikono yao." Rustam aliingiliakati na kuwaomba wasifanye kitu kinyume na matakwa ya balozi.*

*Hata hivyo, baada ya kutafakari Rib'i bin Amir (ra) alishuka juu ya kiti hicho cha kifahari, akapasua sehemu ya zulia kwa jambia lake na kukaa ardhini na kumwambia Rustam, "Hatuhitaji kattu zulia lako. Ardhi iliyokunjuliwa na Mwenyezi Mungu (swt) inatutosha sisi." Rustam kisha akamuuliza Rib'i bin Amir (ra) kupitia mkalimani, "Nini lengo lenu kuandaa vita dhidi yetu?" Rib'i bin Amir (ra) akajibu, "Tuna nia ya kuwaleta watumwa wa Mwenyezi Mungu (swt) katika upana wa maisha yajayo kutokamana na uchache wa maisha haya na kulingania haki na Uislamu kila palipo na mauaji na dini za uongo. Yeyote anayejifunga na haki na Uislamu atatupata sisi hatuingilii katika utajiri wake, mali yake na nchi yake. Lakini tutapigana na yeyote anayetuwekea vikwazo mpaka ima tuingie Peponi au tupate ushindi. Mukitaka kulipa Jizyah, tutaikubali na tutasita kwenda kinyume dhidi yenu na mutatupata tukisimama pamoja nanyi lau na pale ambapo mutakapotuhitaji kwa ajili ya usalama wa maisha na mali zenu." Baada ya kusikia haya Rustam aliuliza, "Wewe ndio mkuu wa Waislamu?" Rib'i bin Amir (ra) alijibu, "La, mimi ni mwanajeshi wa kawaida. Lakini kila mmoja wetu, hata yule aliye kawaida zaidi anaweza kuzungumza kwa niaba ya mtu mwenye nguvu zaidi, na kila mtu ana nguvu kamili katika kila suala."*

*Matamshi ya Rib'i bin Amir (ra) yalimuacha Rustam na waliokuwepo na mshangao mkubwa. Rustam kisha akasema, "uo wa upanga wako umeoza kiasi." Rib'i bin Amir (ra) akautoa upanga wake nje ya uo na kusema, "Lakini umeharibika hivi karibuni tu." Rustam kisha akasema, "sehemu ya makali ya mkuki ni ndogo. Yaweza kuwa na matumizi yoyote katika vita?" Rib'i bin Amir (ra) akajibu, "Hii sehemu ya makali inapenya ndani katika kifua cha adui na kutokeza hadi upande mwingine. Kwani haujaona cheche moja kuwa inatosha kuchoma mji mzima." Baada ya vita hivi vya maneno,*

*Rustam alisema, "Sawa, nitatafakari juu ya matamshi yako na kufanya mkao kutaka ushauri na wanaume wangu walio makini katika kufanya maamuzi." Rib'i bin Amir (ra) alisimama na kurudi kwa Sa'd bin Abu Waqqas (ra).*

*Siku iliyofuata, Rustam alituma ujumbe kwa Sa'd (ra) na kumuomba kutumana balozi kwake. Sa'd (ra) alimtuma Hudhaifah bin Mihsan (ra). Naye pia aliingia katika makao ya Rustam akiwa anamuendesha farasi wake na kuonyesha ushupavu, kama alivyofanya Rib'i bin Amir (ra) hapo awali. Akasogea mbele karibu na kiti cha kifahari akiwa juu ya farasi. Rustam, alisema, "Ni sababu gani umetumwa wewe leo badala ya yule aliyekuja kwangu awali?" Hudhaifah bin Mihsan (ra) akajibu, "Kamanda wetu hufanya uadilifu kwa kila mmoja na humpa fursa kila mmoja kufanya kila kitu. Jana ilikuwa ni zamu yake na leo ni zamu yangu." Rustam kisha akamuuliza, "Munanipa muda gani wa kupumua?" Hudhaifah bin Mihsan (ra) alisema, "Siku tatu pekee kuanzia siku ya leo." Rustam alinyamaza kimya, na Hudhaifah bin Mihsan (ra) akarudi moja kwa moja kwa kambi ya Waislamu. Ushupavu na umakinifu wa akili*

**Endelea... UK 9**

*ya Hudhaifah bin Mihsan (ra) kulimwacha Rustam na waliokuwepo kustaajabu.*

*Siku iliyofuatia Rustam aliomba balozi kutoka kwa kambi ya Waislamu na Mughirah bin Shu'bah (ra) alitumwa kucheza dori yake. Rustam alijaribu vishawishi na vitisho lakini Mughirah bin Shu'bah (ra) hakutishika na kumjibu kwa kama alivyofanya. Kwa kukata tamaa na kuaibika Rustam alisema huku akiwa amejaa hasira, "Sitoingia katika makubaliano aina yoyote nanyi, na nitawaua nyote." Mughirah bin Shu'bah (ra) alisimama na kuondoka kwa amani akielekea katika kambi yake.*

Hayo hapo juu ni taswira ya hali ya Waislamu wanaume wakweli ambao kwamba hii dunia inawahitajia. Wanaume ambao watajituma ili kuishi na kufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa kuitikia mwito wake pale Aliposema, يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱسْتَجِيبُوا۟ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ۖ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ ٱلْمَرْءِ وَقَلْبِهِۦ وَأَنَّهُۥٓ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ **"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa."** [Al-Anfal: 8:24]. Wanaume walio na misheni barabara juu ya hii dunia ya muda mfupi, ambao Mwenyezi Mungu (swt) amewazungumzia kuwahusu, Aliposema, مِّنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا۟ مَا عَـٰهَدُوا۟ ٱللَّهَ عَلَيْهِ ۖ فَمِنْهُم مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُۥ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ ۖ وَمَا بَدَّلُوا۟ تَبْدِيلًا **"Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo."** [Al-Ahzab: 33:23].

Wanaume adhimu walio na malengo watazaliwa, kukuzwa na kulelewa chini ya ngao na mlinzi wa kweli wa wanadamu, Khilafah. Mpaka itakaposimamishwa, tutaendelea kushuhudia majanga duniani kote. Wakati ni sasa kujiunga na mwito ulioshamiri na kutokota wa kuleta MAGEUZI YA KWELI yanayowasilishwa na Hizb ut Tahrir katika machapisho yake yanayofahamika. Usibakie nyuma; muda wetu ni sekunde tu.

Kufanyakazi na Hizb ut Tahrir ni fursa ya kuwa juu ya mzunguko wa kila siku maarufu 'mbio za panya' na kujikwamua kutokamana na kufikiria duni ambako idadi kubwa ya watu ambao wamezama ndani ya uhadaifu na ujinga kwa jina la kuleta mageuzi. Hata hivyo, kiuhalisia sio chochote bali ni kundi la mabawabu wa kisiasa za kisekula za kidemokrasia ambao wapo kwa ajili ya kubakisha hali iliyoko sasa kwa gharama na njia yoyote ile. Hakika, kufanyakazi na Hizb ut Tahrir sio kutembea mbugani kwa wale wanaofahamu ukubwa wa majukumu yake na aina ya kazi zake juu ya mabega yao. Hata hivyo, baada ya wokovu usio na kipimo pale ambapo lengo litatimia katika hii dunia ya muda mfupi na Akhera haidirikiki kattu.

Enyi Wanaume! Tuamkeni, tukazeni mikanda na tupatilize fursa ya kujiunga na kutoa juhudi ya ubora wetu katika mchakato wa kufikia mageuzi msingi. Rizq na ajal zetu HAZIPO katika mikono yetu kwa hiyo hesabu zetu na juhudi zetu kuu zielekezwe katika ulinganizi wa Da'wah. Tuchukue uongozi wa kuziongoza familia, jamii zetu na wanadamu katika nyanja zote za maisha kwa kufanyakazi kwa kujizatiti pasina kuchoka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt) na ilivyoelekezwa na Mtume Wake (saw). Tuweni wanaume walioko hai, makini na mashujaa kimaneno na vitendo.


Pepe: info@uqab.or.ke

JIBU LA SWALI

# Sisi Hatusemi kuwa Habari ya Upokezi wa Mmoja Mmoja (Khabar Ahaad) Ikataliwe, Bali Tunasema Yalazimu Kufanyiwa Kazi

**Swali:**

Assalam Aleykum

Hadithi kubwa zaidi katika Aqida ni Hadith Ahaad, nayo ni Hadith ambayo Jibril alikuja kumuuliza maswali Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), ambapo Mtume alisema: Je, munamjua muulizaji ni nani? Wakasema Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajua zaidi. Akasema: Huyu ni Jibril amekuja kukufunzeni Dini yenu. Hii ni khabar ahaad katika Aqida, basi ni kwa nini tunaikataa?

**Jibu:**

Waaleykum Salaam wa Rahmatullah wa Barakatuh,

Kwanza: Inaelekea hukulidiriki jibu tulilolitoa tarehe 10/09/2022 M kuhusu kuichukulia Hadith kuwa ni dalili katika hukmu za kisharia.Yaani hakulidiriki katika sura yake, sisi hatusemi kuwa khabar ahaad ikataliwe, bali twasema kuwa khabar ahaad ni wajibu kufanyiwa kazi kwayo, lakini haihisabiwi kama dalili ya kukatikiwa katika Aqida, yaani hadith ahaad haitumiwi kama dalili katika Aqida kwa sababu hadith ahaad ni dhanni... Kutochukua Aqida kwa dhana si uzushi, bali iko ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kwani ziko Aya nyingi ndani yake Mwenyezi Mungu anawakemea wale wanaoamini kwa dhana. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمُ الْهُدَى **"Hayo hayakuwa ila ni majina mliyo wapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo. Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa yakini uwongofu ulikwisha wafikia kutoka kwa Mola wao Mlezi."** [An-Najm: 23] Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ لَيُسَمُّونَ الْمَلَائِكَةَ تَسْمِيَةَ الْأُنْثَى * وَمَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئاً **"Hakika wasio amini Akhera bila ya shaka wao ndio wanawaita Malaika kwa majina ya kike. Nao hawana ujuzi wowote kwa hayo isipo kuwa wanafuata dhana tu. Na dhana haisaidii chochote mbele ya haki."** [An-Najm: 27-28] Na akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: وَمَا يَتَّبِعُ أَكْثَرُهُمْ إِلَّا ظَنّاً إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئاً **"Na wengi wao hawafuati ila dhana tu. Na dhana haifai kitu mbele ya haki."** [Yunus: 36] Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ سُلْطَانٍ أَتَاهُمْ كَبُرَ مَقْتاً عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ الَّذِينَ آمَنُوا **"Hao ambao wanajadiliana katika Ishara za Mwenyezi Mungu pasipo ushahidi wowote ulio wafikia, ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya walio amini."** [Al-Ghaafir: 35] Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُمْ بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَاناً **"Na vipi nivikhofu hivyo mnavyo vishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu ambacho hakukiteremshia uthibitisho."** [Al-An'am: 81] na aya zengine nyingi…

Aya hizi ziko wazi katika kuwashutumu wale wanaofuata dhana, na katika kuwashutumu wale wanaofuata bila ya ubainifu, yaani bila ya dalili ya kukatikiwa, na kukemewa kwao na kukashifiwa kwao ni dalili ya katazo la kukatikiwa la kufuata dhana, na katazo la kukatikiwa la kufuata yale ambayo hayakujengwa juu ya dalili ya kukatikiwa... Na kwa sababu aya hizi zimefungika katika masuala ya Aqida, ni makhsusi kwa Aqida... Na yote haya yanaashiria maana ya kukatikiwa kwamba masuala ya Aqida ni lazima yasimame juu yake dalili ya kukatikiwa, vyenginevyo hayazingatiwi, na kwamba haijuzu dalili yake kuwa ya dhana.

Pili: wajibu wa kusimamisha dalili ya kukatikiwa juu ya Aqida ili iwe ni Aqida, na hilo linaashiriwa na Aya zenye hoja zilizo wazi... Hili ni kuhusiana na Aqida.

Ama hukmu za kisheria, inajuzu dalili yake kuwa dhanni, na wala sio sharti kuwa ya kukatikiwa, bali inaweza kuwa dhanni, kwani imethibitika katika andiko la Qur'an Tukufu kwamba inaweza kuhukumiwa kwa ushahidi wa mashahidi wawili, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alihukumu kwa ushahidi wa shahidi mmoja na kiapo cha mwenye haki, na akakubali ushahidi wa mwanamke mmoja katika kunyonyesha, haya yote ni khabar ahaad, na hukmu ni ulazimishaji, na ulazimishaji huu si chochote ila ni ufanyiaji kazi khabar ahaad. Na kuitumia khabar ahaad kama dalili katika kutoa hukmu kama vile kukubali ushahidi na kuhukumu kwa mujibu wake, na yote haya ni katika vitendo, yaani katika hukmu ya Sharia. Na Maswahaba, Mwenyezi Mungu awawie radhi, walikuwa wakikubali maneno ya Mjumbe mmoja katika kuwapa habari kuhusu hukmu ya sharia

kama suala la kuelekea Al-Kaaba (katika swala). Imepokewa na Muslim aliyesema: ametuhadhithia Abdulrahman bin Yusuf aliyesema ametupa habari Malik bin Anas kutoka kwa Abdillah bin Dinar kutoka kwa Abdullah bin Umar amesema: : بَيْنَا النَّاسُ بِقُبَاءٍ فِي صَلَاةِ الصُّبْحِ إِذْ جَاءَهُمْ آتٍ فَقَالَ: إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ قَدْ أُنْزِلَ عَلَيْهِ اللَّيْلَةَ قُرْآنٌ، وَقَدْ أُمِرَ أَنْ يَسْتَقْبِلَ الْكَعْبَةَ فَاسْتَقْبِلُوهَا، وَكَانَتْ وُجُوهُهُمْ إِلَى الشَّأْمِ، فَاسْتَدَارُوا إِلَى الْكَعْبَةِ.. **"Pindi watu walipokuwa katika swala ya asubuhi alikuja my akasema: hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) imemteremkia Quran usiku huu, na ameamrishwa kuelekea Al-Kaaba (katika swala) basi wakaielekea, na nyuso zao zilikuwa zinaelekea Ash-Sham, basi wakaigeukia Al-Kaaba…"**

Na vilevile suala la kuharamishwa pombe, amepokea Al-Bukhari akisema:

***Endelea... UK 11***

Ametuhadithia Yakub bin Ibrahim ametuhadithia Ibn ‘Ulayyah ametuhadithia Abdulaziz bin Suhaib amesema: amesema Anas bin Malik (ra): مَا كَانَ لَنَا خَمْرٌ غَيْرُ فَضِيخِكُمْ هَذَا الَّذِي تُسَمُّونَهُ الْفَضِيخَ، فَإِنِّي لَقَائِمٌ أَسْقِي أَبَا طَلْحَةَ وَفُلَاناً وَفُلَاناً إِذْ جَاءَ رَجُلٌ فَقَالَ: وَهَلْ بَلَغَكُمْ الْخَبَرُ؟ فَقَالُوا: وَمَا ذَاكَ؟ قَالَ: حُرِّمَتْ الْخَمْرُ. قَالُوا: أَهْرِقْ هَذِهِ الْقِلَالَ يَا أَنَسُ. قَالَ: فَمَا سَأَلُوا عَنْهَا وَلَا رَاجَعُوهَا بَعْدَ خَبَرِ الرَّجُلِ). **“Sisi hatukuwa pombe, isipokuwa hii munayoiita al-Fadhikh, na mimi nilikuwa nimesimama namnyesha Abu Talha na fulani na fulani. Akaja mtu akasema: je, imekufikieni habari? Wakasema: Ni nini hiyo? Akasema: Pombe imeharamishwa. Wakasema: Tupa madebe haya ewe Anas. Akasema: Basi hawakuuliza juu yake, wala hawakushauriana baada ya kuambiwa na mtu huyo.”**

**Yote haya hayafanyi kuwepo na shaka yoyote kwamba dalili dhanni inaweza kutumiwa kama dalili katika hukmu ya Sharia.**

Hakika miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu juu yetu ni kwamba ametukataza kuichukua Aqida kwa dhana na akaifanya iwe kwa dalili ya kukatikiwa ili Umma ujumuike pamoja juu yake bila ya kukhitilafiana, kwa hayo Aqida itakuwa safi na takatifu bila ya Muislamu kumkufurisha ndugu yake Muislamu kwa sababu ya kutofautiana kwao katika Hadith dhanni katika Aqida, kwa sababu ikhtilafu katika Aqida ni njia ya kufikia ukafiri, tofauti na hukmu ya Kisharia inayotokana na Hadith ahaad. Ikhtilafu katika hukmu ya Kisharia kihakika sio njia ya kupeleka katika ukafiri. Yeyote anayesema kuwa upanzi shirika (Al-Muzaara’ah) unaruhusiwa kwa sababu ana Hadith ahaad sahih, haimfanyi kuwa kafiri yule anayesema kuwa upanzi shirika ni haramu kwa sababu ana hadith ahaad sahih, na kadhalika... na kwa mlango huu yajuzu kuifanyia kazi hadith ya kukatikiwa na dhanni katika hukmu ya Kisharia na kutochukua hadith dhanni katika Aqida kwa sababu masuala ya Aqida huchukuliwa kutoka kwa yakini.

Pili: Kisha, kutochukua Hadith ahaad katika masuala ya Aqida kulisemwa na magwiji wa wanazuoni wa fiqhi (Fuqaha), kama Imam Abd al-Rahim bin al-Hasan bin Ali al-Asnawi al-Shafi'i, Abu Muhammad, Jamal al-Din. “aliyefariki mwaka 772 H” ametaja katika kitabu chake “Nihaayat al-Sul Sharh Minhaj al-Wasul”: (Na jua kwamba udhihirisho wa dalili ndio njia ya kutokea katika kanuni nyingi za fiqhi, kama vile maelezo ya jumla, khabar ahaad, mlinganisho (qiyas) na ufuatanishi (al-Istaishab), na kadhalika. Wanazuoni wa Usul al-Fiqh, hata wakikubali kufanya kazi nazo, hizo kwao wao sio dalili za fiqhi, bali ni ishara (Amaraat) juu yake. Dalili kwao haitoki isipokuwa kwa lile ilokatikiwa kwayo), wanazuoni wa usul hawazichukulii kuwa ni dalili za fiqhi yaani dalili za hukmu za kisharia kuwa ni dalili, bali wanazichukulia kuwa ni ishara juu ya hukmu za Kisharia, na hiyo ni kwa sababu dalili dhanni hawaichukulii kuwa ni dalili kwao, bali wanaichukulia kuwa ni ishara (Amaarah), kwani dalili kwao haitoki isipokuwa kwa ile iliyokatikiwa kwayo. Hivyo dalili za misingi ya dini lazima ziwe za kukatikiwa (qat’i), na hivi ndivyo alivyosema Ibrahim bin Musa bin Muhammad al-Lakhmi al-Gharnati, maarufu kama al-Shaatibi “aliyekufa: 790 H” katika kitabu chake “Al-Muwaafaqaat”: (Misingi ya fiqhi katika dini ni ya kukatikiwa, si dhanni, na dalili ya hilo ni kwamba inaregea katika ujumla wa Sharia, na kwa sababu ya hivyo, ni ya kukatikiwa... Na lau ingejuzu kuifanya dhanni kuwa asili, katika misingi ya fiqhi, ingejuzu kuifanya kuwa asili katika misingi ya dini, na sio hivyo kwa itifaki. Na vilevile hapa, kwa sababu uwiano wa misingi ya fiqhi na Sharia ni kama uwiano wa msingi ya dini), kwa hivyo anatumia hoja kuwa misingi ya fiqhi ni ya kukatikiwa qat’i), kutokana na umbile lake kama misingi ya dini, na misingi ya dini kwa makubaliano ni ya kukatikiwa (qat’i) , na misingi ya dini ni chimbuko lake ni Aqida, na Aqida ndiyo misingi ya dini... nk

Tatu: Hata hivyo, kuna jambo ambalo ni lazima litiliwe mkazo, nalo ni kwamba maana ya kutoitakidi kwa dalili dhanni haimaanishi kukataa yaliyomo ndani ya Hadith hizi na kutosadikisha yale yaliyokuja ndani yake, bali ni kutoyachukua katika Aqida ambapo Muislamu anamkufurisha ndugu yake Muislamu kwa dhana, na hii ni kutokana na kuwepo mgawanyiko ndani yake... Imekuja katika Kurrasah, ukurasa wa 12 word file: [...kuharamishwa kuitakidi kwa dhanni haimaanishi kukataa yale yaliyomo katika Hadith hizi na kutosadikisha yaliyokuja ndani yake, bali maana yake pekee ni kutoyachukulia kwa mkato (Jazm) yale yaliyomo ndani ya Hadith hizi, lakini yanakubaliwa na kusadikiwa, na yaliyoelezwa ndani yake yanasadikiwa kwa usadikishaji usiokuwa wa mkato. Kilichoharamishwa ni kuitakidi kwayo yaani kwa mkato (Jazm). Bali miongoni mwazo yamekuja maandiko yanayoagiza utendakazi hivyo basi yanatendewa kazi. Kutoka kwa Abu Hurayra amesema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): إِذَا فَرَغَ أَحَدُكُمْ مِنَ التَّشَهُّدِ الأَخِيرِ فَلْيَتَعَوَّذْ بِاللَّهِ مِنْ أَرْبَعٍ، مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ، وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ **“Pindi anapomaliza mmoja wenu Tashahhud ya mwisho, basi naajilinde kwa Mwenyezi Mungu na mambo manne: kutokana na adhabu ya Jahannam, kutokana na adhabu ya kaburi, kutokana na fitina za uhai na mauti, na kutokana na fitina za Masih al-Dajjal”** Imepokewa na Ibn Majah. عن عائشة أن النبي ﷺ كان يدعو في الصلاة: اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَفِتْنَةِ الْمَمَاتِ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْمَأْثَمِ وَالْمَغْرَمِ **“Na kutoka kwa Aisha kwamba Mtume (saw) alikuwa akiomba dua hii katika swala: “Ewe Mola hakika mimi najilinda kwako na adhabu ya kaburi, na najilinda kwako na fitina za Masih al-Dajjal, na najilinda kwako na fitina na uhai na mauti, ewe Mola hakika mimi najilinda kwako kutokana na madhambi na madeni”** imepokewa na Bukhari. Hadith hizi mbili ni khabar ahaad, na ndani yake kuna maombi (talab) ya kitendo, yaani ombi la kuomba dua hii baada ya kumaliza Tashahhud, kwa hivyo ni imependekezwa (Mandub) kuomba kwa dua hii baada ya kumaliza Tashahhud, na yaliyoelezwa ndani yake yanasadikishwa na yanafanyiwa kazi, lakini hayawi ndani ya Aqida maadamu yamekuja katika Hadith ahaad, yaani kwa dalili dhanni, lakini yakija kwa njia ya upokezi wa wingi (Tawatur), basi hapo ni wajib kuyaitakidi...] Mwisho.

Nne: Sasa tunakuja kwenye Hadith ya Jibril (as), iliyotajwa katika swali hili, nayo ni Hadith iliyopokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah na ikapokewa na Muslim na wengineo kutoka kwa Abu Huraira na kutoka kwa Umar Ibn Al-Khattab, ambapo Jibril anamuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kuhusu Uislamu, na akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): الْإِسْلَامُ أَنْ تَشْهَدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّداً رَسُولُ اللَّهِ ﷺ وَتُقِيمَ الصَّلَاةَ وَتُؤْتِيَ الزَّكَاةَ وَتَصُومَ رَمَضَانَ وَتَحُجَّ الْبَيْتَ إِنْ اسْتَطَعْتَ

***Endelea... UK 12***

إِلَيْهِ سَبِيلاً قَالَ: صَدَقْتَ، قَالَ: فَعَجِبْنَا لَهُ يَسْأَلُهُ وَيُصَدِّقُهُ! **"Uislamu ni kushuhudia hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad (saw) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na kusimamisha swala, na kutoa zaka, na kufunga Ramadhan, na kuhiji Makkah kwa mwenye uwezo"** akasema (Jibril): umesema kweli, akasema (Umar): tukamstaajabia, anamuuliza na huku anamsadikisha" قَالَ: فَأَخْبِرْنِي عَنْ الْإِيمَانِ قَالَ: **أَنْ تُؤْمِنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَتُؤْمِنَ بِالْقَدَرِ خَيْرِهِ وَشَرِّهِ** قَالَ: صَدَقْتَ... قَالَ: ثُمَّ انْطَلَقَ فَلَبِثْتُ مَلِيّاً ثُمَّ قَالَ لِي: **يَا عُمَرُ أَتَدْرِي مَنِ السَّائِلُ** قُلْتُ: اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ. قَالَ: «**فَإِنَّهُ جِبْرِيلُ أَتَاكُمْ يُعَلِّمُكُمْ دِينَكُمْ**». Akasema (Jibril): nipe habari kuhusu Iman: akasema (Mtume): **"Ni kumwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Mwisho, na kuamini Qadar kheri yake na shari yake inatoka kwa Mwenyezi Mungu."** Akasema (Jibril): 'umesema kweli'... kisha akaondoka. Kwa hivyo nikasubiri kwa muda, kisha akaniambia (Mtume): **"Ewe Umar je, unamjua muulizaji"** nikasema (Umar): 'Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajua zaidi'. Akasema (Mtume): **"Hakika ni Jibril amewajieni kuwafundisha Dini yenu"**

Hii ni Hadith sahih ambayo haijuzu kukataliwa, na wala haipingani na andiko la kukatikiwa, lakini haitoshelezi kipeke yake kuwa dalili katika Aqida... Hata hivyo, jumla ya mambo ya Aqida yaliyomo ndani yake yamekuja katika dalili nyenginezo za kukatikiwa (qat'i). Kwa hivyo nguzo za imani zimetajwa na aya tukufu za Qur'an, na pia nguzo za Uislamu... Hivyo basi, yote yaliyotajwa katika Hadith hii ni mambo ambayo yamebainishwa kwa dalili nyenginezo za kukatikiwa zisizokuwa Hadith hii, hivyo yanachukuliwa katika Aqida kwa dalili zake za kukatikiwa, kama vile kauli ya Mwenyezi Mungu (swt):

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا آمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَى رَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي أَنْزَلَ مِنْ قَبْلُ وَمَنْ يَكْفُرْ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالاً بَعِيداً**

**"Enyi mlio amini! Muaminini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Kitabu alicho kiteremsha juu ya Mtume wake, na Kitabu alicho kiteremsha kabla yake. Na anaye mkataa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Akhera, basi huyo amekwisha potelea mbali."** [An-Nisaa: 136] na akasema Mwenyezi Mungu (swt):

**آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ**

**"Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni kwako."** [Al-Baqara: 285]

Vivyo hivyo, kuamini Qadar kwa maana ya elimu ya Mwenyezi Mungu na kuandikwa katika Ubao Uliohifadhiwa (Al-Lawh al-Mahfudh). Amesema Mwenyezi Mungu (swt): **قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً** [At-Talaq:...] **وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ قَدَراً مَقْدُوراً** [Al-Ahzab:...] **مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ**. **كَانَ ذَلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُوراً** [Al-Isra:...]. Hakuna kinachotokea isipokuwa kwamba kilikwisha kadiriwa na Mwenyezi Mungu, na kimeandikwa ndani ya Kitabu, yaani isipokuwa kimetanguliwa na elimu ya Mwenyezi Mungu, hivyo Qadar ni kinaya kwa elimu ya Mwenyezi Mungu, kama ambavyo Kitabu ni kinaya kwa elimu ya Mwenyezi Mungu. Na kwa hiyo, Qadar katika Sharia maana yake ni kile kilichotanguliwa na elimu ya Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo maana yake kama ilivyoelezwa katika maandiko ya Qur'an na maandiko ya Sunnah.

Na vilevile nguzo za Uislamu ziko katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu:

**فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوَاكُمْ**

**"Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa."** [Muhammad: 19]

**مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ تَرَاهُمْ رُكَّعاً سُجَّداً يَبْتَغُونَ فَضْلاً مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَاناً**

**"Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu."** [Fat'hi: 29]

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ**

**"Enyi mlio amini! Mmefaradhishiwa Saumu, kama ilivyo faradhishwa kwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu."** [Al-Baqara: 183]

**وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ**

**"Na shikeni Swala, na toeni Zaka, na inameni pamoja na wanao inama."** [Al-Baqara: 43]

**وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلاً**

**"Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea."** [Aal-i-Imran: 97]

**Hivyo basi Hadith hii haikataliwi bali hufahamiwa kwa sura yake kama ilivyo bainishwa hapo juu**

Nataraji kwamba sasa imekuwa wazi.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**11 Jumada al-Awwal 1444 H**
**05/12/2022 M**